

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA



TAARIFA KWA UMMA

Katibu wa Bunge anautaarifu Umma wa Watanzania kuwa amepokea nakala ya barua kutoka kwa Mhe. Job Y. Ndugai, Mb. ya kujiuzulu nafasi ya Spika wa Bunge aliyompelekea Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi (CCM) ambacho kilimdhadini alipogombea nafasi hiyo.

Aidha, amepokea barua kutoka kwa Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi (CCM) iliyomtaarifu kuwa Mhe. Job Y. Ndugai, Mb. amejiuzulu nafasi ya Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuanzia tarehe 06 Januari, 2022 na kwamba Chama hicho kimeridhia.

Taarifa kuhusu taratibu za uchaguzi kwa ajili ya kujaza nafasi ya Spika zitatolewa baadaye.

Imetolewa na:

Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano wa Kimataifa,
Ofisi ya Bunge,
DODOMA.

06 Januari, 2022